halotel

*Dar es Salaam,* March 15th 2021

COMMISSIONER GENERAL
TANZANIA REVENUE AUTHORITY,
P. O. Box 11491
DAR ES SALAAM

Dear Sir,

**RE: SUBMISSION OF HALOTEL'S OPINIONS AS PER MEETING HELD ON 10th MARCH, 2021**

Reference is made to the above heading and to your E-mail with reference title. **MAOMBI YA HALOTEL YANAYOHUSU KURUDISHIWA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI KIASI CHA TZS 10,211,190,143.15**

We Viettel Tanzania PLC, we received an e-mail from TRA official requesting us to go through the minutes of meeting which was held at TRA head office on 10th 03 2021 under you and then handed over to Deputy Commissioner of Large Tax Payer Department.

After review of the enclosed file, we found that some of our key points were not included in the minutes of meeting which was sent to us; and so we decided to do the changes to accommodate our points and send to TRA for updating the previous one. On March 15th 2021 we received again the same minutes (without any changes as per our proposal) from TRA official which was signed by all TRA participants.

Our opinions are based on the fact that the accounting errors were due to weakness of our accounting and finance department having graduates fresh from colleges at that time. We Viettel Tanzania PLC. (Halotel) didn't intend to misreport, also TRA took the money that wasn't theirs considering our company didn't lodge any refund of VAT in that particular time. PCA department request confirmation from Large Tax Department about our VAT position for the company, and the request was forwarded to investigation department of which it didn't do any investigation rather than look into time frame which was elapsed on our side and agency notice was issued towards us without any investigation. Under sections 39, 40, 41 and 45 of Tax Administration Act, gives power to Commissioner General to review and accept refilling of VAT after a written formal request from tax payer of which on 04th September 2019 we wrote a letter requesting to adjust our VAT balance and it was accepted on 03rd October 2019 to rectify the balance with appropriate relevant evidences and documents.

In light of the above and in view of further improving good relationship and cooperation between Viettel Tanzania PLC and your office, we kindly request your esteemed office to reconsider and

Viettel Tanzania Public Limited Company
Address:10th Floor, Tanzanite Park Building, P.O.Box 34716, DSM, Tanzania
Website: Halotel.co.tz Email: Info@halotel.co.tz

Scanned with CamScanner

have a neutral team if necessary which shall handle the matter for the purpose of providing fair judgment for both parties. HALOTEL request a fully refund of TZS, 10,221,190,143.15 by cash continue its operations smoothly.

It's our sincere hope that our request will be considered.

Thank you,

**FOR AND ON BEHALF OF VIETTEL TANZANIA PLC**

VIETTEL TANZANIA PLC
P. O. Box 34716
DAR ES SALAAM
52674

**MR. NGUYEN TIEN DUNG**
**ACTING MANAGING DIRECTOR**



Scanned with CamScanner

**MAREKEBISHO YA RIPOTI YA PAMOJA YA KIKAO BAINA YA TIMU YA WATAALAM WA MAMLALA YA MAPATO TANZANIA (TRA) NA WAWAKILISHI WA KAMPUNI YA M/S VIETTEL TANZANIA PUBLIC LIMITED COMPANY (HALOTEL) KILICHOFANYIKA MNAMO TAREHE 10 MACHI 2021**

---

**SOMO: MAOMBI YA HALOTEL YANAYOHUSU KURUDISHIWA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI KIASI CHA TZS 10,211,190,143.15**

---

**AGENDA**

1. Kufungua Kikao
2. Majadiliano
3. Kufunga Kikao

## 1. UTANGULIZI

Kikao hiki cha Wataalam kilifanyika kufuatia kikao cha ufunguzi chini ya Mwenyekiti, Dr. Edwin P. Mhede, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mnamo tarehe 10 Machi 2021 muda wa saa 4.00 asubuhi.

Kikao cha ufunguzi kilianza kwa Kamishna Mkuu kutoa nafasi kwa Wataalam na Wawakilishi kutoka kampuni ya HALOTEL kueleza wajumbe wa kikao madhumuni ya kuomba kikao. Wawakilishi wa HALOTEL walielezea kwa ufupi kuwa malalamiko yao yalihusu kutokujibiwa kwa barua zao walizowasilisha Idara mbalimbali za TRA wakiomba kurudishiwa kiasi cha TZS 10,211,190,143.15 kilizochukuliwa na TRA kwenye akaunti za kampuni kwenye benki nne tofaouti kwa kutumia Hati ya Uwakala (Agency Notice).

Wawakilishi hao walieleza kuwa baada ya kiasi cha fedha kilichotajwa hapo juu kuchukuliwa kwenye akaunti, kampuni ilishindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi, kulipia manunuzi vipuri kwa ajili ya mitambo ya kampuni na kushindwa kulipia huduma mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa kila siku wa kampuni na pia kupelekea kupunguza baadhi ya wafanyakazi na tatizo hilo (kusindwa kujiendesha kiufanisi) linaendelea kuikabili kampuni mpaka sasa. HALOTEL ilimwandikia barua Kamishna wa walipakodi wakubwa mnamo tarehe 4 Septemba 2019 yenye kumb. Na. HALOTEL/HQ/026/09/2019 inayohusu kufanya marekebisho ya ritani ya kodi ya ongezeko la thamani kutoka nje ya nchi (VAT on imports) ya nyuma (Mei 2015)



Scanned with CamScanner

iliyokosewa, Barua hii ilijibiwa na Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa barua yenye Kumb.Na.104-967-116 ya mnamo tarehe 3 Octoba 2019, ambayo ilikubali maombi ya HALOTEL kufanya marekebisho ya ritani ya kodi iliyokesewa (Mei 2015) ndani ya mwezi Octoba 2019 ikiwa na viambatanisho vyote muhimu, ikiwemo ushahidi wa mabadiliko hayo. Wataalam wa TRA walieleza mbele ya Kamishna Mkuu kuwa, kwa ufahamu wao, kesi ya kampuni hiyo ilitokana na ukaguzi uliofanyiwa kampuni hiyo na Kitengo cha Post Clearance Audit (PCA) ambacho kiko chini ya Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa. Ukaguzi uliofanyika ulihusu bidhaa zote zilizoingizwa nchini kutoka nje ya nchi na kampuni ya HALOTEL kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari 2014 hadi Desemba 2018. Aidha, ukaguzi uliofanyika uligundua kuwa kampuni ya HALOTEL ilizidisha kiwango cha ritani ya kodi (over-claim) ya ongezeko la thamani kutoka nje ya nchi (VAT on Imports) kuliko ilivyoonekana katika mfumo wa ushuru wa forodha (TANCIS) kwa TZS, 10,895,500,253.4. Kiasi hiki cha kodi kinajumuisha TZS 10,221,190,143.15 – *overclaimed VAT on imports*, TZS 379,602,844.34 - *VAT on other charges* na TZS 294,707,266 - *misclassification*. Kampuni ya HALOTEL ilikubali na kulipa kiasi cha TZS 674,310,110.30 kilichotokana na *VAT on other charges* na *missclasification.*

Baada ya kulipa TZS, 674,310,110.30, HALOTEL ilieleza kwamba kiasi cha 10,221,190,143.15. ambacho kilionekana kama overclaim kilisababiswha na makosa katika ritani ya kodi ya mwezi wa 5, 2015 na si makosa ya kodi iliyolipwa katika forodha hivyo ilipendendekeza kwenye ripoti ya ukaguzi kuwa, PCA wawasiliane a Kitengo cha Walipa Kodi Wakubwa kujua salio la kodi ya ongezeko la thamani inayopaswa kulipwa HALOTEL (VAT Refundable) na iweze kupunguza kiwango hicho kwa TZS, 10,221,190,143.15 kutoka kwenye salio la ziada ambalo mpaka Juni 2019 lilikuwa TZS, 72,921,346,551.73.

Pia, HALOTEL walitarajia uwepo wa masaliano baina ya Idara za ndani za TRA (PCA na LTD) kuweza kujiridhisha na kujua kiwango halisi cha kodi ya ongezeko la thamani kinachopaswa kulipwa kwa kampuni ya HALOTEL ili kipunguzwe kutoka kwenye overclaimed VAT on imports ya mwaka 2015. Matokep yake hakukuwa na mawasiliano thabiti baina ya idara tajwa na hivyo kupelekea kufungwa kwa akaunti nne tofauti za benki (CRDB Bank, BOA Bank, SCB Bank na NMB Bank) za kampuni ya HALOTEL na kusababisha kampuni kushindwa kujiendesha kw ufanisi kwa kipindi chote hicho ilhali tulikuwa na ongezeko la ziada la thamani ambalo lingeweza kupunguzwa kama kungekuwa na mawasiliano mazuri ya idara tajwa za TRA.

Kupitia kikao cha Machi 10, 2021, Kaimu Kamishna wa PCA alisema kulikuwa na mawasiliano ya ndani ya idara tatu za TRA (PCA, LTD na Investigation) ambazo kwa pamoja zilishauriana na kukubaliana kutoa hati ya uwakala (Agency Note) bila kufanya uchunguzi kwa mapendekezo yetu ya kupunguza kiasi cha TZS, 10,221,190,143.15 kutoka kwenye salio letu chanya (ziada) 72,921,346,551.73. (mpaka Juni 2019) linalopaswa kulipwa kwa kampuni ya HALOTEL, Idara ya



Scanned with CamScanner

ukaguzi ya TRA haikufanya uchunguzi kama ilivyotakikana kwa kigezo cha muda kuwa ulikuwa umepita hivyo hakukuwa na sababu ya kufanya uchunguzi, mantiki hii HALOTEL inaamini haikutendewa haki kwa kufungiwa akaunti zake za benki pasi na uchunguzi kufanyika.

Baada ya kushindwa kupata kielelezo cha kuthibitisha kuwa Idara ya Walipakodi Wakubwa ilikubali kuondoa deni la TZS 10,221,190,143.15 kwenye kiasi cha *refund* waliyokuwa wanadai, Idara ya Forodha ilimwandikia Waraka wa Ndani Kamishna wa Idara ya Walipakodi Wakubwa kupata uthibitisho kama kweli walikubaliana na ombi la kampuni ya HALOTEL. Baada ya kupokea Waraka wa Ndani, Kamishna wa Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa kuzingatia kuwa HALOTEL ilikuwa ikifanyiwa uchunguzi alimwomba Kamishna wa Upelelezi wa Kodi kuchunguza madai ya HALOTEL kwamba kiasi cha TZS 10,221,190,143.15 ambacho kampuni inadaiwa ililipwa kinyume na taratibu ilitokana na makosa ya kibinamu wakati wa kujaza ritani na kurekodi.

Baada ya kupitia maombi ya kampuni, Kamishna wa Upelelezi wa Kodi alibaini kuwa kampuni ya HALOTEL ilishindwa kuwasilisha maombi ya kurekebisha ritani ndani ya kipindi cha miaka mitatu (3) inayotakiwa kwa mujibu wa Kifungu cha 66(3) cha Sheria ya Ongezeko la Thamani, SURA 148. Kwa hiyo, alishauri Idara ya Forodha ichukue hatua stahiki kudai kodi ya TZS 10,221,190,143.15 ambayo kampuni ilikuwa inadaiwa. Baada ya kupata maelekezo haya, Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa ilizielekeza Benki za CRDB BANK PLC, STANDARD CHARTERED BANK TANZANIA LIMITED, BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED, na NMB BANK PLC, kulipa kodi iliyokuwa inadaiwa kutoka kwenye akaunti za kampuni ya HALOTEL, kwa mujibu wa Sheria.

Baada ya kusikiliza mawasilisho ya HALOTEL, kwa upande mmoja, na baada ya kuwa amewasikiliza Watumishi wa TRA, kwa upande mwingine, kuhusiana na hoja zilizowasilishwa na HALOTEL, Kamishna Mkuu alielekeza kuwa ni busara kuwe na majadiliano jumuifu ya kiufundi na ya kina kwa lengo mahususi la kujielimisha zaidi kwa ufasaha juu ya maombi ya HALOTEL ili yeye aweze kushauriwa ipasavyo, kiufundi, na kwa kuzingatia misingi ya Sheria. Hivyo, alielekeza pande zote mbili wajadili kwa pamoja na kukubaliana kwa pamoja ushauri wa namna ya kupata suluhisho la changamoto ilioyojitokeza.

## 2. MAJADILIANO YA KIUFUNDI

Mnamo tarehe 4 September 2019 kampuni ya HALOTEL iliwasilisha barua kitengo cha walipakodi wakubwa kuomba kufanya marekebisho ya ritani zake kodi zilizokesa Mei, 2015 yenye thamani ya TZS, 10,221,190,143.15. HALOTEL ilikubaliwa kufanya marekebisho hayo ndani ya Mwezi wa kumi, 2019.



Scanned with CamScanner

Wataalam waliohudhuria kikao kutoka TRA, wanaamini barua tajwa haikuwa na uhusiano na makosa ya ritani ya kodi ya ongezeko la thamani yaliyotokea Mei 2015 bali ilikuwa ni ruhusa ya marekebisho ya mwezi wa kumi, 2019, ambapo kwa kipindi hicho hakukuwa na makosa yanayohusiana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT on imports). Pia, walikubaliana kwa pamoja hata kama maombi haya yalipokelewa yasingeweza kufanyiwa kazi kwa sababu yaliwalishwa nje ya muda unaotakiwa kisheria kwa Kifungu cha 66(3) cha Sheria ya Ongezeko la Thamani, SURA 148.

Kupitia kwa mwanasheria wa Kampuni ya HALOTEL ambaye pia alikuwa ni mjumbe wa kikao husika, alipendekeza mambo yafuatayo;

*"Si kweli kwamba tulikubaliana hakuna nafasi ya kisheria, Mwanasheria wetu alinukuu kifungu namba 39 cha sheria ya uthibiti wa kodi (Tax administration act) ambayo inatoa nguvu ya kisheria kwa kamishna mkuu wa TRA kuruhusu kufanya upya marekebisho ya ritani za kodi kutatua makosa yaliojitokeza kipindi cha nyuma"*

*"Pia ieleweke makosa haya yalifanyika May 2015, TRA ilichukua pesa waliyoiona imedaiwa kimakosa na Halotel hivyo kuirejesha pasi kujiridhisha kama TRA iliwalipa Halotel hiyo pesa, hivyo walichukua kisicho chao, kwani TRA wanajua hawajalipa madai yoyote ya kodi ya ongezeko la thamani kwa kampuni ya HALOTEL kuanzia mwaka 2014 hadi 2019 hata kama hakukuwa na maombi ya malipo hayo kutoka kampuni ya HALOTEL."*

*"PCA wanakiri hawakujibiwa na idara ya walipa kodi wakubwa walipouliza kama HALOTEL imewahi kulipwa madai ya Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) au kuwa na salio chanya katika ritani za kodi tajwa, badala yake Idara ya ukaguzi wa kodi ya TRA waliwashauri PCA kutoa hati ya uwakala kama jibu la swali la PCA kwa Idara ya walipa kodi wakubwa, Tunafikiri kitengo cha uchunguzi cha TRA hakikupaswa kuwajibu PCA badala yake ingewajibu Idara ya walipa kodi wakubwa, swali hilo la PCA lilijenga msingi wa kitaalam ambao ungeweza kuepuka usumbufu huu uliojitokeza, Idara ya uchunguzi ya TRA (Investigation Department) kuwajibu PCA tunaamini haikuwa sawa"*

*"Makosa haya ya kihesabu yalitokana na udhaifu wa Idara yetu ya uhasibu kwa kipindi hicho kuwa na wafanyakazi wahitimu kutoka chuo, hivyo kukosa uzoefu na kupelekea kujitokeza kwa makosa tajwa na si kwalengo la kuiba mapato ya serikali"*

Baada ya wajumbe kujadili kwa kina wataalam kutoka TRA walisisitiza ya kwamba ombi la kampuni ya HALOTEL halitekelezeki kwa sababu ya changamoto ya sheria ya Ongezeko la Thamani Sura Na. 148 kifungu 66(3) ambacho kina ukomo wa muda wa miaka 3 kupita kama kigezo. Hii ni kwa sababu baada ya kupewa barua



Scanned with CamScanner

ya madai, kampuni ya HALOTEL ilipendekeza kupunguzwa kwa kodi hiyo katika salio lake la ziada lakini Matokeo yake 10,211,190,143.15 ilichukuliwa kutoka kwenye akaunti zake za benki nne tofauti. Aidha, wataalamu wa kodi wa TRA walisisitiza ya kwamba, kampuni ya HALOTEL haikupinga makadirio ya kodi kwa Kamishna Mkuu, ikiwa ni kwa mujibu wa Kifungu cha 51 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438. Kutokana na changamoto ziliyojitokeza. Wataalam wa HALOTEL wanamwomba Kamishna Mkuu kutumia kifungu Na. 40, 41 na 45, cha sheria ya usimamizi wa kodi kinachompa uwezo wa kuruhusu marekebisho ya ritani za kodi ya ongezeko la thamani kutatua changamoto inayoikabili kampuni ya HALOTEL. Ili iweze kurejeshewa kiasi TZS 10,221,190,143.15 kilichochukuliwa kwenye akaunti za kampuni. Vilevile, ielewek endapo hawatarejeshewa kiasi hicho cha fedha wanazodai, kampuni itashindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi, kulipa fedha ya kununulia vipuri kwa ajili ya mitambo yake, na kushindwa kulipa gharama mbalimbali za uendeshaji wa kampuni za kila siku na hivyo kufunga biashara zake hapa nchini.

## 3. MAPENDEKEZO YA KIKAO

Kampuni ya HALOTEL, inaamini kwamba makosa yaliyofanyika ya kutuma ritani za kodi ya ongezeko la thamani kwa makosa kwa mwezi mei, 2015 hayastahili adhabu ya kuchukua kiasi chote TZS, 10,221,190,143.15 pasi na kwamba hakuna marejesho yeyote yale ambayo kampuni ya HALOTEL imeomba na kulipwa kwa kipindi chote kuanzia mwaka 2015 mpaka 2019 kuhusiana kiwango chanya cha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ilichokuwa nacho hadi Juni 2019. Hivyo kampuni ya HALOTEL inaomba kurudishiwa kiasi cha TZS, 10,221,190,143.15 kwa pesa taslimu.

Pia tunaamini ya kwamba kosa lililofanyika lilistahili onyo la maandishi kwa sababu katika kipindi chote hatukawahi kufanya kosa kama hilo au kurudia kosa.

## 4. KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao kwa kuwashukuru wajumbe wote kwa michango waliyotoa kwenye kikao ambayo imewezesha kufikia uelewa wa pamoja wa kuhusiana na maombi tajwa ya HALOTEL. Aidha, Mwenyekiti aliahidi kusambaza muhtsari wa kikao kwa Wataalam wa pande zote mbili kwa ajili ya kusainiwa ili sasa nay eye aweze kuwasilisha kwa Kamishna Mkuu kwa ajili ya ufahamu wake na pengine, ikionekana inafaa kwa kuzingatia Sheria, naye aweze kufanyia kazi mapendekezo yaliyobainishwa kwenye taarifa hii.

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa sita na robo mchana.



Scanned with CamScanner

**WALIOHUDHURIA**

| Na. | JINA | KAMPUNI | WADHIFA | SAHIHI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mr. Herbert Kabyemela | TRA | Mwenyekiti | |
| 2 | Mr. Narcis Lumumba | TRA | Katibu | |
| 3 | Mr. Finias M. Gatawa | TRA | Mjumbe | |
| 4 | Mr. Joseph Mtalemwa | TRA | Mjumbe | |
| 5 | Mr. Tran Ngoc Hoi | HALOTEL | Mjumbe | |
| 6 | Mr. Nguyen Van Khanh | HALOTEL | Mjumbe | |
| 7 | Mr. Lustoy Mfaume | HALOTEL | Mjumbe | |
| 8 | Mr. Akbar Mohamed | HALOTEL | Mjumbe | |
| 9 | Mr. Nahshon Bohela | HALOTEL | Mjumbe | 16/03/2021. |



Scanned with CamScanner